EAST AFRICAN
CRUDE OIL
PIPELINE

# Mpango Kazi wa EACOP na Jamii za Pembezoni Zinazojitambua Kama Watu wa Asili Tanzania

16t Septemba 2022

ZERO HARM
KAZI BILA MADHARA

# Mpango Kazi wa EACOP na Jamii za Pembezoni Zinazojitambua Kama Watu wa Asili Tanzania

16 Septemba 2022

# YALIYOMO


Mpango Kazi wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili........3

1. Utangulizi........3
2. Misamiati.........3
3. Dhumuni........4
4. Dhamira ya EACOP........4
   a. kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa........5
   b. Kujengeana-uwezo........8
   c. Mwenendo wa Usimamizi wa Malalamiko........9
   d. Kushughulikia madhara yanayoweza kujitokeza........11
   e. Faida za Mradi........15
   f. Kushirikiana na Serikali.........16
5. Uwezeshaji wa Utekelezaji wa Mpango wa EACOP.........17
   a. Uwezeshaji wa EACOP........17
   b. Uwezeshaji wa Asasi za Kiraia (NGOs)........17
   c. Uwezeshaji wa Viongozi wa mila........17
6. Tathmini na Ukaguzi wa Utekelezaji........17
   a. Tathmini kwa njia ya ushiriki na mijadala........18
   b. Tathmini ya Mwisho wa Mwaka........19

Randama A: Wasifu wa Jamii........20

Randama B: Nyaraka Rejea........21

# Mpango Kazi wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili.

## 1. Utangulizi

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ni bomba la mafuta ghafi lenye urefu wa Kilometa 1,443 litakalosafirisha mafuta ghafi kutoka Kabaale-Hoima nchini Uganda hadi rasi ya Chongoleni karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania. Mradi wa EACOP unaendelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi na vigezo vya kimataifa kuhusu tija katika biashara, vikiwemo vigezo vya Kampuni ya Fedha ya Kimataifa (IFC) kuhusu mazingiria na jamii, pamoja na dira za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu. Kwa kuzingatia hilo, EACOP imeridhia Sera ya Haki za Binadamu inayohusu kujiwajibika katika haki za binadamu na umakini, pamoja na kuheshimu haki za binadamu za Makundi ya Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa, yaani Wa-Maasai, Wa-Akie, Wa-Barbaig na Wa-Taturu.

Mpango Kazi huu wa wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (Mpango Kazi wa EACOP) ni sehemu ya msingi kuhusu namna ambavyo EACOP ina shughulikia madhara yanayotokana na Mradi yanayoweza kutokea katika Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, kwa kuzingatia mila na desturi zao Pamoja na kuhesimu vigezo vya kitaifa na kimataifa kuhusu haki za binadamu, vikiwemo Vigezo namba 7 vya IFC kuhusiana na watu wa Asili.

Mpango huu wa EACOP umepatikana kutokana na umakini na ushirikishwaji kambambe na ambao bado unaoendelea kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, mashirika yasiyo ya kiserikalli, wataalam wa kitaifa na wa Kimataifa na wadau wengine tangu mwaka 2017. Mpango huu umeundwa katika msingi wa Mfumo wa EACOP wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (Mfumo wa EACOP) iliyo ridhiwa na kutiwa sahihi na EACOP Pamoja na viongozi wa mila wa jamii tajwa hapo yaani wa-Maasai, wa-Akie, wa-Bargaig Pamoja na wa-Taturu Octoba 2021.

## 2. Misamiati.

Kufuatia ushirikishwaji wa wataalam wa kitaifa na viongozi wa mila wa jamii husika, EACOP imeridhia kutumia msamiati "Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili" ikimaanisha jamii za kitanzania ambazo zinakidhi vigezo vya kimataifa katika kutambulika kama Watu wa Asili.

Kwa Mujibu wa Umakini wa Mradi hadi sasa, Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanaoguswa na Mradi ni pamoja na Wa-Maasai, Wa-Akie na Wa-Datoga (wakijumuisha Wa-Barbaig na Wa-Taturu).

## 3. Dhumuni

Dhumuni la Mpango Kazi wa EACOP ni kufafanua dhamira ya Mradi wa EACOP na utekelezaji wake ili kuimarisha uzingatiaji wa Haki za Binadamu, utu na mila na desturi za Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanaoguswa na Mradi.[1]

Mpango wa EACOP unafafanua zaidi kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa EACOP ambao ulisainiwa na EACOP pamoja na viongozi wa mila wa-Maasai, wa-Akie, wa-Taturu na Wa-Barbaig. Uliandaliwa kulingana na tafiti mbalimbali na ushirikishwaji wa wataalam wa kitaifa na kimataifa na mashirika yasiyo ya kiserikali (Asasi za Kiraia (NGOs)) ambayo yana aminiwa na jamii husika.

Mpango wa EACOP na Mfumo wa EACOP zina tazamiwa kufikia vigezo na matakwa mahususi ya kigezo cha IFC namba 7 kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili na misingi na mifano bora ya Ushirikishwaji na Upashanaji Habari wenye Tija (ICP) na Ushirikishwaji mpana wenye uelewa kabla ya kutekelezwa kwa Mradi (FPIC).

## 4. Dhamira ya EACOP

Dhamira ya EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili watakao guswa na Mradi imejikita katika maeneo makuu sita yafuatayo ambayo yalikubaliwa awali katika Mfumo wa EACOP na yanafafanuliwa zaidi katika Mpango Huu.

(a) kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa

(b) kuwezesha kujengeana uwezo;

(c) kuwezesha namna ya utatuzi wa Malalamiko unaozingatia mila na desturi;

(d) kushughulikia madhara yatokanayo na uendelezaji wa Mradi wa EACOP.

(e) kuchochea maendeleo na manufaa kwa jamii kwa namna inayoheshimu mila na desturi; na

(f) kushirikiana na serikali kadri itakavyo hitajika.

[1] Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanaweza kuguswa katika ujenzi na uendeshaji wa shughuli za bomba la mafuta na miundo mbinu mingine, pamoja na mnyororo wa thamani wa mahusiano ya kibiashara ya Mradi. Madhara hayo yali ainishwa katika Tathmini ya Haki za Binadamu (HRIA), Pamoja na tafiti zingine kama vile Tathmini ya Mazingira na Jamii (ESIA) na Mikakati wa Uhamishaji (RAPs). Madhara hayo yatapitiwa upya katika mpango wa ushirikishwaji wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili unaoendelea kwa sasa, Pamoja na taarifa za mara kwa mara za HRIA na tathmini ya utekelezaji wa Mipango ya usimamizi wa Mazingira na Jamii pamoja na Mipango ya Uhamishaji wa Watu na Makazi (RAPS).

Ufuatao ni ufafanuzi wa utekelezaji wa dhamira kama ilivyo ainishwa hapo juu.

### a. kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa

EACOP inadhamiria kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa (ikifahamika pia kama ICP) kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili kwa maana ya viongozi wa mila, viongozi wa jamii, wanajamii watakao guswa na Mradi, na wana kaya watakao guswa na Mradi.

EACOP inatambua kwamba kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa ni jambo linaloendelea kwa sasa na endelevu na EACOP ime andaa mpango kabambe wa ushirikishwaji kwa ngazi ya viongozi wa mila na katika ngazi za jamii kama inavyofafanuliwa hapa chini.

#### *Mikutano ya Mara nne kwa mwaka na Viongozi Kimila*

EACOP imedhamiria kuandaa mikutano ya Mara nne kwa mwaka na Viongozi wa mila wa Ki-Maasai, Ki-Akie, Ki-Barbaig na Ki-Taturu. Viongozi waalikwa kutoka katika jamii hizo watajumuisha pia viongozi wa kike pamoja na wanawake Maarufu wa jamii husika.

Kwa ujumla, mikutano hii ya mara nne kwa mwaka huwa na sura ya warsha ambayo inapokezana kati ya mikutano maalum ya jamii husika ya kila kundi katika eneo la karibu na kwao, na mkutano mkuu wa makundi yote tajwa katika eneo moja.

Kwa ujumla warsha hufanyika kwa siku 3 kama ni mkutano wa jamii zote kwa ujumla na siku mbili kama ni kwa jamii moja peke yake. Warsha pia zitatoa fursa ya faragha kati ya viongozi wa mila na Asasi ya Kiraia (NGO) ili kuhakikisha kwamba taarifa zinazotolewa zina eleweka na kwamba mrejesho wa EACOP unawasilishwa vyema kwa wahusika.

Pamoja na kwamba kuna nafasi ya makubaliano kwamba lini hasa mikutano ya mara nne kwa mwaka ifanyike, EACOP na viongozi wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wamedhamiria kukutana mara nne kwa mwaka ili kutekeleza Mpango wa EACOP. Mikutano ya ziada inaweza kuitishwa kama ikionekana inafaa.

#### *Ushirikishwaji katika ngazi za jamii*

EACOP pia imedhamiria kuwa na mikutano ya mara nne kwa mwaka na viongozi na wanajamii (wakijumuisha wanawake, vijana na wawakilishi wa wazee) wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanao guswa na Mradi, hususan kama kuna uwezekano wa kuwepo kwa madhara katika ardhi zinazomilikiwa na jamii kwa ujumla na maeneo yenye umuhumu wa pekee kwa mila na desturi.

Ushirikishwaji katika ngazi za wana jamii umeundwa kwa kuzingatia majukwaa shirikishi yanayo zingatia mila na desturi, yaliyopendekezwa na viongozi wa mila na viongozi wa jamii, na ambayo yanafaa katika kuwasilisha taarifa ya majadiliano katika ngazi za jamii. Majukwaa hayo pia yataratibu utatuzi wa Malalamiko kama inavyofafanuliwa katika sehemu ya 4(c) hapa chini.

Pamoja na kwamba majukwaa ya ushirikishwaji katika ngazi za jamii yanakubalika katika kila jamii husika, kuna mfanano wa majukwaa yanayotumika na kila Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili kama jedwali na. 1 hapa chini linavyo onesha.

## Jedwali na. 1: Muhutasari wa majukwaa ya ushirikishwaji wa ngazi ya wana jamii.

| Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili | Majukwaa ya ushirikishwaji wa wana jamii yanayozingatia mila na desturi |
|---|---|
| Wa-Akie | Kamati ya wana jamii na kamati ya Wazee |
| Wa-Maasai | Kamati ya Viongozi wa Mila na Baraza la Wanawake |
| Wa-Barabaig | Baraza la Wazee |
| Wa-Taturu | Baraza la Wazee |

Ushirikishwaji wa ngazi ya wana jamii pia unahusisha mikutano maalum midogo na vikundi vya mijadala na wazee, wanawake na wasichana, vijana na makundi mengine madogo katika jamii husika. EACOP itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Asasi za Kiraia (NGOs) ili kufahamu mapendekezo yao kuhusu ushirikishwaji wa jamii unaozingatia mila na desturi.

Maelezo ya kina ya majukwaa ya ushirikishwaji na namna ushirikishwaji utakavyo fanyika katika jamii husika, upo katika Wasifu wa kila jamii katika Sehemu ya Pili na Mpango huu wa EACOP.

## *NGO na Msaada wa Kitaalam kuhusu Ushirikishwaji unaoendelea*

Ushirikishwaji unaoendela unawezeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yana aminiwa na viongozi wa mila na jamii kwa ujumla na ambayo yana utaalam au ubobezi katika kutekeleza haki za Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili Tanzania. Mashirika hayo ni Pamoja na Pastoralist Indigenous Non-Governmental Forum (PINGOs Forum), Parakuiyo Pastoralists Indigenous Community Development Organisation (PAICODEO) na Ujaama Community Resources Team (UCRT).

Kama inavyo ainishwa katika kipengele cha sita hapa chini, EACOP ime andaa hati ya makubaliano (MoU) na Asasi za Kiraia (NGO) husika ambayo inaelezea namna ya uwezeshaji wao kwa mujibu wa Mfumo wa EACOP na Mpango wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. Nakala ya MoU hiyo imejumuishwa katika Sehemu ya Tatu ya Mpango huu wa EACOP.

## *Uratibu wa Ushirikishwaji*

Ajenda ya Mkutano mmoja kati ya Mikutano Minne kwa Mwaka, itatokana na mrejesho au "yatokanayo" na mkutano uliopita kabla ya mkutano husika. Ajenda zitajumuisha pia mapendekezo ya mada zinazohitajika na watoa mada husika (kwa mfano Watumishi wa EACOP, Wataalam wanaohusishwa na tafiti mbali mbali za Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili nakadhalika), Ili kupashana Habari na kujengeana uwezo kwa namna inayozingatia mahitaji na maombi ya viongozi wa asili na viongozi wa jamii.

Ajenda na mahali mkutano utakapofanyika, vitajadiliwa na viongozi wa mila na Asasi za Kiraia (NGOs) kama sehemu ya ufungaji wa mkutano unaoendelea kwa wakati huo. Taarifa itatolewa kabla ya muda kwa viongozi wa mila, viongozi wa jamii, na NGO husika kuhusu ratiba na madhumuni ya mkutano unaotarajiwa kufanyika.

## *Maudhui ya Ushirikishwaji*

Kwa Ujumla, mikutano ya ushirikishwaji wa viongozi wa mila, viongozi wa jamii, na wanajamii itakuwa na maudhui yafuatayo:

- Ushirikishwaji utahusisha mrejesho wa shuguli za EACOP kwa ujumla na shughuli mahususi zinazohusu eneo la jamii husika.
- Ushirikishwaji utahusisha mrejesho huhusu tathmini za mazingira na jamii na tafiti zingine zinazohusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili.
- Ushirikishwaji utatoa mrejesho kuhusu ajira za wananchi na mikataba ya ajira ili kuwezesha wana jamii kuzijua fursa zilizopo.
- Ushirikishwaji utahusisha mrejesho kuhusu utekelezaji wa Mpango wa EACOP kwa ujumla na majibu kuhusu maombi ya maelezo ya ziada yatokanayo ya kikao kilichopita.

## *Tafsiri*

Nyaraka maalum zinazo husiana na Mradi, kama vile Mfumo wa EACOP na Mpango Kazi wa EACOP vimetafsiriwa kwa Kiswahili kama lugha ya Taifa la Tanzania, pia imekubalika kwamba Kiswahili ndiyo lugha ya kipaumbele ambayo kwayo, nyaraka za EACOP zitakuwa zikitafiriwa. Vile vile, tafsiri katika Ki-Maasai na Ki-Barbaig zitafanyika kulingana na maombi ya wana jamii husika. Juhudi bora za makusudi zitafanyika kutafsiri nyaraka maalum kwa Ki-Akie.[2]

Mbadala wa kutumia nyenzo za Sauti na picha katika kutafsiri hukubalika kama nanma bora ya kupashana habari na kuwasiliana miongoni mwa wana Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili.

[2] Kuna watu wachache ambao bado wanazungumza ki-Akie, hata miongoni mwa wa-Akie wenyewe. Hivyo basi, kutakuwa na changamoto kuwapata wataalam wa kutafsiri na hivyo kuna haja ya kutumia namna mbadala za sauti na picha katika kutafsiri kwa lugha ya ki-Akie.

Wakalimani wanao aminika watahudhuria mikutano ili wana Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili waweze kutumia lugha zao bila matatizo kuwasiliana na Mradi.

*Wawakilishi wa Serikali*

Wawakilishi wa Serikali kwenye Mradi wa EACOP katika ngazi ya Wilaya (DFPs) katika Mradi na wawakilishi wengine wa serikali wanaweza kuhusishwa katika ushirikishwaji wa viongozi wa mila na viongozi wa jamii wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili ili kuhakikisha kwamba wana uelewa mpana kuhusu utekelezaji wa Mpango Kazi wa EACOP ili wawezeshe utekelezaji wake kama itakavyo onekana inafaa. Maelezo ya ziada ya ushirikishwaji wa Serikali yanapatikana katika kifungu cha 4(f) hapa chini.

*Uhuru wa kutotishiwa*

Ushirikishwaji wa ngazi ya jamii utakuwa huru dhidi ya aina yoyote ya vitisho ambavyo vinaweza kuwa vizuizi vya ushiriki wenye uelewa mpana wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. EACOP itajibu na kushughulikia mara moja, kwa msaada wa Asasi za Kiraia (NGOs) na washauri kutoka nje au wataalam kama itakavyo onekana inafaa, tuhuma zote za matisho ama ulipizaji kisasi kuhusiana na mradi wa EACOP.

## b. Kujengeana-uwezo

Mradi unawawezesha na kuwajengea uwezo wana jamii wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanaoguswa na Mradi, ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika Mradi kwa namna yenye uelewa mpana na kwa usawa. Muundo wa Ushikishwaji na Ushiriki wenye uelewa mpana unao endelea kwa sasa unao jumuisha warsha ya siku 2 hadi 3 mara nne kwa mwaka, ume asisiwa ili kutoa fursa kwa namna endelevu ya kujengeana uwezo.

Vipaumbele vya ujengaji uwezo huibuliwa na viongozi wa mila na huhusisha pia nia ya kutafsiri na kuandika kwa lugha rahisi, majarida yanayohusu Mradi ili kuwawezesha katika jukumu lao la kuwapasha habari na kuwashirikisha wana jamii. Hivyo basi, EACOP hutafsiri kwa Kiswahili nyaraka muhimu zinazohusiana na Mradi, Mfumo wa EACOP na Mpango Kazi wa EACOP (na kwa lugha nyingine kama itakavyo hitajika) na kuwezesha kuwepo kwa wakalimani wanao aminika kufanikisha mpango wa kujengeana-uwezo.

Vilevile EACOP hualika wazungumzaji (kama vile Wafanyakazi wa EACOP, wataalam waliohusika katika tafiti mbalimbali za Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, na kadhalika) kuwezesha ujengaji wa uwezo kuhusu Mradi na taratibu zake mbalimbali za kusimamia na kupunguza madhara ya kimazingira, kijamii na haki za binadamu. Mijadala inayo endelea na Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili Pamoja na Asasi za Kiraia (NGOs) wakati wa mikutano minne ya mwaka hutumika kuibua mada zinazohitajika na pande zote kwa ajili ya ujenzi wa uwezo katika mkutano unaofuata. Kama ilivyo oneshwa hapo juu, kipaumbele kitatolewa katika

kuhakikisha mada zitakazojadiliwa zina tija kwa wanawake viongozi wa mila na wanawake mashuhuri wanaohudhuria mikutano husika. Nyenzo za ujenzi wa uwezo (kama vile nyenzo za mawasiliano au mawasilisho ya EACOP kutoka kwa watoa mada waalikwa) hutolewa kwa viongozi wa mila ili kuwawezesha kuwasilisha katika ngazi za jamii.

Vilevile, viongozi wa mila wame omba kuwezeshwa katika Nyanja ya usafiri ili kuwasaidia kufikisha ujumbe kwa wana jamii na kupata mrejesho. Mradi huwawezesha viongozi wa jamii kutoka maeneo yote yanayo guswa na Mradi, kushiriki katika mikutano ya mara nne kwa mwaka ili kuwezesha kupashana habari katika ngazi ya jamii. Uwezeshwaji wa ziada kwa viongozi wa mila kukutana na wana jamii katika ngazi za jamii utafikiriwa na EACOP kama swala la mtu binafisi au hitaji la mtu mmoja mmoja na litaratibiwa na NGO-husika ama na Mratibu wa EACOP (CRC).

## c. Mwenendo wa Usimamizi wa Malalamiko

### *Mwenendo wa EACOP wa Usimamizi wa Malalamiko*

Mradi Umeandaa Mwenendo wa Usimamizi wa Malalamiko kuwezesha usimamizi na utatuzi wa Malalamiko inayohusisha wanajamii.[3]

Ili kuhakikisha Mwenendo wa Mradi wa Usimamizi wa Malalamiko una endana na mila na desturi, Mradi uli shirikisha Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili na Mradi umerekebisha Mwenendo huo kwa kuzingatia maoni hayo kama inavyo onekana katika jedwali hapo chini.

Majukwaa ya wana jamii yanayo fanikisha mchakato wa Ushirikishwaji na Ushiriki wenye uelewa mpana kama ulivyo fafanuliwa katika kifungu cha 4(a) hapo juu na katika Wasifu wa jamii kama zinavyosomeka katika Sehemu ya Pili ya Mpango huu wa EACOP zitajengewa uwezo wa kupokea Malalamiko kutoka kwa wana jamii na kuwasilisha kwa Mradi, pia watashiriki kutatua Malalamiko mapema kwa kutumia majadiliano, usuluhishi na mila na desturi kama itakavyo onekana inafaa.

Jedwali na. 2: Nukuu kutoka katika Mwenendo wa EACOP wa Usimamizi wa Malalamiko ya Jamii

| **2.6. Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili** |
|---|
| Mradi wa EACOP utazigusa moja kwa moja ama bila kuzigusa moja kwa moja Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, yaani Wa-Maasai, Wa-Akie na Wa-Datoga (Wa-Barbaig na Wa-Taturu). Jamii hizi zinapatikana katika Wilaya za Handeni na Kilindi Mkoani Tanga, Kiteto, Simanjiro na Hanang Mkoani Manyara, Kondoa Mjini Mkoani Dodoma na Igunga Mkoani Tabora. Makundi haya yanahitaji ushirikishwaji na umakini Maalum kutokana na upekee wa Maisha yao, na makazi yao yaliyoko pembezoni mno na utegemezi wao wa uoto wa asili.<br><br>EACOP huwatendea kwa usawa watu wote wanao guswa na Mradi kulingana na upekee wao na tofauti za kimila na desturi. Kwa Muktadha wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili Mfumo wa EACOP wa Usimamizi wa Malalamiko umejumuisha wawakilishi wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, Kamati zao za uhusiano wa jamii (yaani mabaraza) |

[3] Mwenendo wa EACOP wa Usimamizi wa Malalamiko, Kumb. Na. L2-STO-TZ-0136

na viongozi wa mila watakapo hitajika kufanikisha usimamizi wa malalamiko katika jamii yao. Hupewa namba maalum za kupiga kukiwepo na malalamiko katika jamii zao na viongozi husaidia kutafsiri. Kuwepo kwa wawakilishi wa jamii husika ni muhumu kwakuwa watu wengi wa jamii husika hupenda kuwa wazi na kutoka ushirikiano kwa/ama wakiwepo watu wanao waamini kutoka katika jamii zao.

Katika Mwenendo Huu wa Usimamizi wa Malalamiko, EACOP imejumuisha dhamira yake ya Usimamizi wa Malalamiko kama ilivyo ainishwa katika Mfumo wa EACOP wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (Mfumo wa EACOP ) ambayo ili asisiwa na kukubaliwa kupitia mchakato wa ushirikishwaji wa viongozi wa mila, wana jamii na wawakilishi wa NGO zinazo wakilisha Jamii za Pembezoni Zinazojitambua a kama Watu wa Asili.

Mfumo wa EACOP una ainisha yafuatayo:

- Ili Kuhakikisha kwamba Mwenendo wa Usimamizi wa Malalamiko una endana na mila na desturi, Mradi ulishirikisha Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili na uta rekebisha Mwenendo huo kufuatana na maoni yaliyotolewa.
- Majukwaa ya Ushirikishwaji jamii (kama yalivyokubalika kwa ajili ya Ushirikishwaji na Ushiriki wenye Uelewa Mpana katika kifungu kidogo cha (a) cha Mfumo wa EACOP, pia yata jengewa uwezo ili kupokea Malalamiko yanayohusu Mradi kutoka kwa wana jamii, kuwasilisha taarifa kwa EACOP na kusaidia utatuzi wa malalamiko kwa haraka kwa njia ya majadiliano, usuluhishi na mila na desturi kama itakavyo onekana inafaa.
- Juhudi za pamoja za Mradi, Asasi za Kiraia (NGOs) na majukwaa ya jamii katika kufanikisha mwenendo wa utatuzi wa Malalamiko katika ngazi ya jamii zitazingatia elimu ndogo ya baadhi ya wana jamii, haja ya kurahisisha Mwenendo wa Malalamiko na matumizi ya mila na desturi kama itakavyo hitajika.
- Utoaji taarifa na ushirikishwaji endelevu kuhusu umadhubuti wa Mwenendo wa Utatuzi wa Malalamiko katika ngazi ya jamii utafanyika katika mikutano minne ya mwaka inayohusisha viongozi wa mila na viongozi wa jamii.
- EACOP na Uongozi wa mila umekubaliana kumteua mwakilishi kutoka katika moja ya Asasi za Kiraia (NGOs) zinazo saidia shughuli za EACOP kushauri na kutatua tatizo lolote linalotokana na utekelezaji wa Mfumo wa EACOP kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, Mpango wa EACOP Kuhusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili ama Ushirikishwaji wenye Uelewa Mpana ama FPIC (kama itakavyo hitajika).

Yafuatayo yatazingatiwa endapo Malalamiko husika yatahusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili:

- Mawasiliano kwa njia ya mazungumzo na mkalimani ni muhimu kwa kuwa wana jamii kutoka katika makundi haya wanaweza wasielewe Kiswahili ama wanapenda kutumia lugha zao za asili.
- Mlalamikaji anaweza kusindikizwa na mwakilishi wa jamii yake.
- Katibu wa jamii ama timu ya EACOP yaweza kumsaidia mlalamikaji katika kujaza fomu ya malalamiko wakati wa kusajili ama kufunga lalamiko.

Juhudi za Pamoja za EACOP, Asasi za Kiraia (NGOs), viongozi wa mila na majukwaa ya wanajamii kudumisha uelewa kuhusu Mwenendo wa Usimamizi wa Malalamiko wa ngazi ya jamii, utazingatia ukweli kwamba baadhi ya wana jamii wana elimu ndogo, haja ya kurahisisha mwenendo na matumizi ya mila na desturi kama itakavyo hitajika. Mradi ume andaa na kutafsiri miongozo ya Usimamizi wa Utatuzi wa Malalamiko ili kuongeza uelewa katika ngazi za jamii. Miongozo hii imeambatanishwa katika randama B cha Mpango kazi huu wa EACOP.

Utoaji wa taarifa na ushirikishwaji endelevu kuhusu umadhubuti wa Mwenendo wa Utatuzi wa Malalamiko katika ngazi ya jamii utafanyika katika mikutano minne ya mwaka inayohusisha viongozi wa mila na viongozi wa jamii.

### *Uwezeshaji wa Asasi za Kiraia (NGOs) katika Utatuzi wa Malalamiko*

Mradi na Viongozi wa mila wamekubaliana kumteua mwakilishi wa PINGOs Forum kusaidia katika kushauri na kutatua Malalamiko inayotokana na utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

Majukumu ya Mwakilishi wa PINGOs Forum yataamuliwa kwa kuzingatia tukio husika ila yaweza kujumuisha yafuatayo:

- Kutoa ushauri wa utatuzi wa Malalamiko kwa kuzingatia mila na desturi na dhamira yenye kutenda haki kwa wanajamii kutokana na Malalamiko ambayo hayakuweza kutatuliwa kupitia usuluhishi na wanajamii.
- Kuwezesha mijadala na usuluhishi kati ya EACOP na viongozi wa mila ama viongozi wa jamii kuhusu Malalamiko ama mambo mengine yahusuyo utekelezaji wa Mpango wa EACOP.
- Kupendekeza wataalamu wa kuwezesha upatikanaji wa ukweli na namna nyingine za utatuzi wa Malalamiko ili kusaidia kutatua Malalamiko na mambo mengine yatokanayo na utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

## d. Kushughulikia madhara yanayoweza kujitokeza

Mradi una dhamira ya kushughulikia madhara yote yatakayo wapata mtu mmoja mmoja na wana jamii wote, ikiwa ni pamoja na Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. Dhamira hiyo ni pamoja na:

- Utekelezaji wa mpango wa mazingira, jamii na haki za binadamu ulio andaliwa kwa Mradi mzima kwa njia ya tathmini ya Madhara ya Mazingira na Jamii (ESIA), tathmini ya madhara ya Haki za Binadamu (HRIA) pamoja na mpango wa Uhamishaji Makazi (RAPs). Hujumuisha mpango wa kuboresha Maisha ya watu walioguswa moja kwa moja na Mradi, wakiwemo wana Jamii za pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili.
- Kuweka vipaumbele katika jitihada za kupunguza madhara, ama kuunda namna ya upunguzaji wa madhara utakao zuia ama kupunguza madhara kwa wana Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. Haya yatafanyika kwa kuwashirikisha wana Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili na wawakilishi wao.
- Mbinu za kimkakati na za ziada za kupunguza madhara ziliibuliwa wakati wa kuandaa wasifu wa jamii na zimeambatanishwa kama sehemu ya Pili ya Mpango huu wa EACOP.

## *Madhara ya kimkakati na jinsi ya kuyapunguza.*

Jedwali lifuatalo linaainisha kwa ufupi madhara ya kimkakati ambayo yaliibuliwa kupitia kwa Mpango wa Mradi kujitathmini kiumakini, na kwa njia ya ushirikishwaji wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. Ikiwa ni Pamoja na uandaaji wa wasifu wa jamii na ushirikishwaji wa ziada ili kuelezea madhara ya mradi katika Nyanja ya Tathmini ya Madhara ya mazingira na Jamii. Utambuzi wa madhara haya ya kipaumbele utatumika kuwezesha utoaji wa taarifa na ushirikishwaji pamoja na kujengeana uwezo unaoendelea kwa jamii, kuhusu namna Mradi utakavyo punguza na kushughulikia madhara. Utambuzi huo pia utasaida katika kupima na kusimamia utekelezaji wa wakandarasi watakao tekeleza Mradi wakati wa ujenzi wa bomba.

Jedwali C: Madhara yanayopewa kipaombele na namna ya kuyakabili

| Aina ya Madhara | Madhara makubwa | Namna ya kuzikabili na kushughulikia |
|---|---|---|
| Madhara ya kimila na urithi | • Madhara yanayoweza kutokea katika maeneo ya kuabudia, yanayotumika kwa mikutano na sherehe za kimila na kiroho (mfano engigwana kwa wa-Maasai)<br>• Madhara yanayoweza kugusa maeneo mengine ya kukutania yenye umuhimu wa kimila.<br>• Madhara yanayoweza kugusa makaburi ama sehemu zingine zenye umuhimu wa ki-ibada. | • Ushirikishwaji, utambuzi na uchambuzi wa maeneo ya kuabudia ya wana jamii.<br>• Makubaliano ya FPIC yamefikiwa na jamii ya wa-Akie kuhusiana na madhara katika eneo la kuabudia na Makubaliano mengine ya FPIC yatafikiwa kuhusiana na maeneo mengine ya kuabudia ambayo hayakuwekwa wazi hapo awali.<br>• Kufanikisha uhamishaji wa maeneo ya kuabudia na sherehe za matambiko[4]<br>• Ushirikishwaji kuhusu jitihada za ziada zitakazo tekelezwa na wakandarasi wakati wa ujenzi kuhusiana na maeneo yote ya kiutamaduni yaliyoko karibu na maeneo ya ujenzi.<br>• Kupindisha bomba pale inapowezekana kuepusha madhara katika sehemu za urithi wa asili. |
| Madhara yanayohusiana na ardhi | • Madhara yanayoweza kugusa ardhi ya asili inayotumika kama nyanda za malisho. | • Mchakato wa utwaaji wa ardhi na urejeshaji wa fursa za kiuchumi unaozingatia sheria za Tanzania na IFC PS 5. |

[4] Rejea: Cultural Heritage Management Plan and CCPs; Ethnographic Study.

| Aina ya Madhara | Madhara makubwa | Namna ya kuzikabili na kushughulikia |
|---|---|---|
| | • Madhara yanayoweza kugusa ardhi ya vijiji inayotumika na wanajamii.<br>• Madhara yanayoweza kugusa ardhi zinazomilikiwa na watu binafsi, ikiwa ni pamoja na rasilimali kama vile mazao na miti.<br>• Madhara yanayoweza kuathiri vyanzo vya maji yanayotumika na binadamu na mifugo.<br>• Madhara yanayo weza kuathiri mali asili ya misitu (inayotumika kutengeneza asali ama kwa ajili ya dawa na vyakula vya asili.)<br>• Madhara katika nyumba na miundo mbinu mingine. (ikiwa Pamoja na vivuko vya wakati maalum kama masika ama kiangazi. | • Ulipaji fidia kwa haki na uwazi na kuwahusisha wana ndoa wote.<br>• Urejeshwaji wa fursa za kiuchumi unaundwa na kuzingatia Maisha na uzalishaji mali wa jamii husika.<br>• Kuwapo kwa nyumba mbadala kwa kaya zenye sifa.<br>• Urejeshwaji wa vyanzo vya maji kwa kaya zenye sifa.<br>• Ushirikishwaji katika kutambua maeneo ya vivuko na kujenga vivuko vya muda na kuhakikisha uwepo wa washika vibendera [5]. |
| Madhara mengine kwa jamii | • Madhara yanayoweza kutokea kwenye afya, na usalama kutokana na muingiliano wa wafanyakazi-ikiwa ni pamoja na hofu ya madhara kwa wanawake yanayotokana na uhamiaji ama uwepo wa wafanyakazi wakati wa ujenzi wa bomba.<br>• Madhara yanayoweza kutokana na uwepo wa magari mengi na ajali.<br>• Madhara ya mifugo kushindwa kufika katika sehemu za kunywa maji na madhara yanayoweza kutokana na kuwepo kwa mitaro.<br>• Madhara yanayoweza kutokana na hisia za kutotendewa haki katika ulipaji wa fidia kwa rasilimali zinazomilikiwa kwa ujumla ama stahiki ambazo | • Kushirikiana na serikali za mitaa kuhakikisha uwepo takwimu za awali kuhusu afya katika vijiji vilivyo athiriwa.<br>• Kuandaa warsha kukuza uelewa wa maswala ya afya kwa wana jamii.<br>• Kutoa elimu ya usalama barabarani na kuweka alama zinazo eleweka katika tamaduni husika.<br>• Jitihada mahususi kuhakikisha uwepo wa fursa za ajira kwa wana jamii (Tazama Kifungu cha 4(e) hapa chini.[6] |

[5] Rejea: Resettlement Action Plans and CCPs, including Livelihood Restoration Plan and Vulnerable Peoples' Plans; Natural Resource Management Plan and CCPs; Biodiversity Management Plan and CCPs; Pollution Prevention Plan and CCPs; Community Health, Safety and Security Management Plan and CCPs.

[6] Rejea: EACOP Code of Conduct; Community Health, Safety and Security Management Plan and CCPs; Transport and Road Safety Management Plan and CCPs; Procurement and Supply Chain Management Plan and CCPs; Labour Management Plan and CCPs; Project-Induced In-Migration Plan and CCPs; Stakeholder Engagement Plan and CCPs.

| Aina ya Madhara | Madhara makubwa | Namna ya kuzikabili na kushughulikia |
|---|---|---|
| | kisheria zinapelekwa vijijini na siyo katika vitongoji ambapo makundi ya wana jamii wa pembezoni wanaishi.<br>• Uwezekano wa wanajamii (hususan vijana na wanawake) kuwa na changamoto ya kupata fursa za ajira kutokana na kutopata habari ya fursa hizo kwa wakati ama kutokuwa na sifa zinazo hitajika. | |
| Madhara kwa wanawake | Madhara yanayoweza kutokea kwa wanawake kwa kutoruhusiwa kumiliki ardhi, mifugo ama mali na hivyo kuathiri stahiki zao katika fidia na madhara mengine.<br>• Madhara yanayoweza kutokea kwa wanawake kwa kutoruhusiwa kuongea mbele ya jamii na kutoa mawazo katika kufikia maamuzi.<br>• Uwezekano wa wanaume kutumia vibaya fedha za fidia.<br>• Ugumu kwa wanawake kunufaika na Mradi kwa njia ya ajira au miradi ya maendeleo. | • Kukuza uelewa kwa wana jamii kuhusu haki za wanawake kumiliki ardhi, mifugo na mali zingine.<br>• Uandaaji wa mikutano mahususi ya wanawake peke yao wakati wa kupashana habari na ushirikishwaji.<br>• Kuwatumia wanawake mashuhuri na wanao aminika kutoa taarifa kuhusu fursa za ajira. [7] |

## *Makubaliano ya Ridhaa Huru ya Uelewa (FPIC)*

Pamoja na kwamba Mpango wa EACOP ni kuwezesha msingi wa Ridhaa Huru ya Uelewa (FPIC) kwa Jamii zote za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. EACOP inatambua kwamba FPIC itahitajika kwa shughuli maalum na madhara kwa baadhi ya jamii kwa mujibu wa Kigezo namba 7 cha International Finance Corporation (IFC) kinachohusu Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (yaani madhara yanayotokana na kuhamishwa na athari kwenye rasilimali zinazotumika ama Kumilikiwa kimila na madhara katika urithi na maeneo ya kuabudia). Uwezekano huo umetambuliwa kwa njia ya utafiti na ushirikishwaji wa viongozi wa jamii na mila. Ridhaa Huru za Uelewa zinazohitajika zimeambatanishwa katika Sehemu ya Pili ya Mpango huu wa EACOP, ikiwa ni Pamoja Wasifu wa Jamii.

[7] Rejea: Ethnographic Study, Resettlement Action Plans and CCPs, including Livelihood Restoration Plan and Vulnerable Peoples' Plan, Stakeholder Engagement Plan and CCPs and Labour Management Plan and CCPs.

## e. Faida za Mradi

Mradi unawezesha manufaa kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili wanao guswa na Mradi kwa namna inayo zingatia ukweli kwamba Mradi ni wa wawekezaji binafsi na rasilimali zilizopo zitumike kuchochea maendeleo kwa jamii nzima inayoguswa na Mradi.

### *Fursa za ajira*

Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili zimeeleza uhitaji wao wa fursa za ajira kwa wanajamii wao. Pia wameelezea baadhi ya vikwazo wanavyo kutana navyo katika kupata ajira kutokana na umbali wa ki-jeografia, lugha, kiwango cha elimu na mambo mengine.

EACOP itawezesha majadiliano kati ya wataalamu wa fursa kwa wazawa, viongozi wa mila, viongozi wa jamii na NGO ili kuweka mikakati ya kupambana na changamoto za kupata ajira kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili.

Vilevile EACOP itawasiliana mapema na wakandarasi ambao watakuwa katika maeneo ya Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili ili kuwahimiza umuhimu wa kutoa ajira kwa wana jamii wa jamii hizi kwa kuepuka ubaguzi dhidi yao.

Dhamira ya EACOP kuweka mazingira ya upatikanaji wa fursa za ajira utajumuisha:

- Mahudhurio ya mara kwa mara ya wahusika wa Kitengo cha Fursa kwa Wazawa katika mikutano ya mara nne kwa mwaka na viongozi wa asili ili kutoa mrejesho na fursa tarajiwa pamoja na mambo ya kujifunza kutokana na jitihada za kuajiri katika maeneo mengine.
- Kuandaa mikutano na Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili ili kuwa elezea fursa zinazo tarajiwa na taratibu za ajira kabla ya kuanza kwa shughuli za ujenzi wa bomba katika maeneo yao.
- Kuwaalika wakandarasi ambao watatoa ajira kwa wenyeji kuhudhuria mikutano ya mara nne kwa mwaka na viongozi wa mila na mikutano mingine ya jamii kabla ya kuanza kwa ujenzi katika maeneo yao ili kuwezesha upashanaji wa habari kuhusu taratibu za ajira zinazotarajiwa.
- Kutoa taarifa kwa wakati kuhusu fursa za ajira kwa wanajamii kwa njia ya (a) Kubandika matangazo ya ajira katika maeneo yanayo fikika na kukubaliwa na wanajamii na (b) Kuwajulisha viongozi wa mila pamoja na wana vikundi (kama ilivyo oneshwa katika kifungu cha 4(a) hapo juu. Maelezo mengine kuhusu namna ya kuwasilisha taarifa za sifa za ajira katika ngazi ya jamii yanapatikana katika wasifu wa jamii katika Sehemu ya 2 ya Mpango wa EACOP.

### *Uwekezaji katika Jamii*

Katika dhamira yake ya kuchochea manufaa ya kiuchumi, EACOP itatekeleza Mpango wa Uwekezaji katika Jamii mahususi kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili. Kadri itakavyo wezekana, uwekezaji huo utadhamiria kuchochea manufaa ya kiuchumi kwa wana jamii kwa ujumla na utakuwa ni nyongeza kwa fursa za ajira na jitihada zingine kama vile urejeshwaji wa mbinu za kupata mahitaji ambayo kwa kawaida hulenga mtu mmoja mmoja ama kaya iliyopo katika jamii iliyo athiriwa na Mradi.

Dhamira ya EACOP katika uwekezaji wa manufaa ya jamii ni pamoja na:

- Kuchagua shirika (kampuni ama Asasi ya Kiraia (NGO)) kuunda na kutekeleza mradi wa uwekezaji katika jamii kwa Jamii ya Pembezoni Inayojitambua kama Watu wa Asili.
- Muundo wa mradi wa uwekezaji katika jamii utajikita katika kuimarisha uzalishaji mali wa asili wa Jamii ya Pembezoni Inayojitambua kama Watu wa Asili ikiwa ni Pamoja usimamizi wa ardhi, afya na usimamizi wa mifugo na mahitaji rasmi ya wanawake.[8]
- Muundo wa mradi wa uwekezaji katika jamii utakuwa na sura mtambuka, ikijumuisha maswala ya matakwa ya uhifadhi na maendeleo endelevu na utatekelezwa kwa namna shirikishi kwa kuzingatia maoni ya viongozi wa mila, pamoja na wanawake na vijana. Pia utazingatia maoni ambayo yamesha kusanywa kutoka kwa viongozi wa mila na wana jamii kwa njia ya maandalizi ya wasifu wa jamii kama inavyo oneshwa katika Sehemu ya 2 ya Mpango wa EACOP.
- Baada ya uundaji kukamilika, mkakati kamili wa utekelezaji wa mradi wa uwekezaji wa manufaa kwa jamii utawasilishwa na kuwashirikisha viongozi wa mila na wana jamii katika mikutano mikuu ya mwaka na vikao vingine vya jamii.
- Mkakati wa Utekelezaji utajumuisha mkakati wa vigezo vya kupima na kutathmini utekelezaji wa mpango wa uwekezaji wenye manufaa kwa jamii, ambao utatumika sambamba na mkakati wa tathmini katika Sehemu ya 6 hapa chini.
- Mkakati wa Kutathmini pia utajumuisha mahitaji ikiwa ni pamoja na mchango ya kifedha na usio-wa kifedha kutoka EACOP, pamoja na mkakati wa kuongeza rasilimali zingine za kiserikali, za binafsi ama za NGO ili kukuza manufaa ya kimaendeleo na mradi wa uwekezaji wenye manufaa kwa jamii.

## f. Kushirikiana na Serikali.

EACOP imedhamiria kutumia nafasi yake ya kimkakati pamoja na washirika wake katika biashara na pande nyingine husika, kama vile wawakilishi wa serikali, kushughulikia madhara yanayoweza kujitokea na katika kufanikisha uwekezaji wenye manufaa ya kijamii kwa Jamii za Pembezoni zinazojitambua kama Watu wa Asili.

Hususan, EACOP inawezesha serikali za mitaa kuhakikisha zinajumuisha wana jamii wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili katika mijadala ya madhara ya Mradi hususani katika maeneo ambayo wana Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili ni wachache.

Sehemu na jinsi ya kuwawezesha wana jamii wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili umeainishwa katika Wasifu wa Jamii katika Sehemu ya Pili na Mpango Kazi wa EACOP.

---

[8] EACOP imekamilisha mchakato wa Maombi ya kuonesha nia mnamo tarehe 24 Agosti, 2022 na imeanza hatua nyingine ya mchakato wa kufanya chaguzi kupitia kuomba mapendekezo ya utekelezaji. Ikiwa shirika bora limebainishwa, muundo wa mpango wa Uwekezaji katika Jamii utatakiwa kuanza katika theluthi ya mwisho yam waka 2022.

Mapendekezo muhimu ya kupunguza madhara na faida za kijamii yanaendana na sheria za Tanzania na mikakati ya serikali. Hususan, ugawaji ardhi Tanzania kwa mujibu wa sheria, unalenga kupunguza Malalamiko ya ardhi na kutenga maeneo ya ardhi ya vijiji kwa ajili ya nyanda za malisho na shughuli za kiutamaduni.

Vilevile, vipaumbele vya kushirikiana na serikali katika kupunguza madhara na kuwezesha manufaa katika ngazi ya jamii vimeainishwa katika Wasifu wa Jamii kwenye Sehemu ya Pili ya Mpango huu wa EACOP. Vile vile, Muundo wa Mradi wa Uwekezaji katika kijamii utaendana na miradi mingine ya serikali na mashirika mengine.

Kuhusu ushirikishwaji unaoendelea wa serikali kuhusu utekelezaji wa Mpango wa EACOP, wawakilishi wa serikali (DFP) hualikwa katika mikutano yote minne ya mwaka na viongozi wa mila na mikutano mingine ya ngazi za jamii. Vile vile, wawakilishi wengine wa serikali katika ngazi za vijiji, kata na wilaya hualikwa kwenye mikutano ama warsha kama inavyo hitajika ili kuhakikisha wana elewa Mradi na kuomba ushirikiano wao katika utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

## 5. Uwezeshaji wa Utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

### a. Uwezeshaji wa EACOP

EACOP itatoa uwezeshaji utakao hitajika kutekeleza shughuli zitakazo kubalika kahusiana na mpango huu wa EACOP, ikiwa ni Pamoja na muda wa wafanyakazi wake, uwezeshaji wa vifaa na fedha. Hii ita jumuisha pia uwezeshaji unao endelea wa Mtaalam wa Kitanzania wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili na Mshauri wa Kimataifa wa Haki za Binadamu.

### b. Uwezeshaji wa Asasi za Kiraia (NGOs)

EACOP imeandaa hati maalum ya ushirikiano (MoU) na PINGOs Forum, PACOIDEO na UCRT kuwezesha utekelezaji wa Mfumo wa EACOP na Mpango wa EACOP. Mbali na MoU hiyo, EACOP pia imesaini mkataba na kila NGO na inaandaa mpango kazi wa utekelezaji wa Mpango wa EACOP.

### c. Uwezeshaji wa Viongozi wa mila

Viongozi wa mila wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili pia watawezesha utekelezaji wa Mpango wa EACOP kwa njia ya kushiriki katika Mikutano minne ya mwaka na kuwezesha jitihada za Mradi za kutoa taarifa na kushirikisha viongozi wa jamii na wana jamii kwa ujumla.

## 6. Tathmini na Ukaguzi wa Utekelezaji

Ili kuwezesha utekelezaji Madhubuti wa Mpango wa EACOP, shughuli zifuatazo za tathmini na ukaguzi zitafanyika kulingana na uundwaji shirikishi wa vigezo vya utekelezaji (KPI) baina ya viongozi wa mila na NGO kuhusiana na sehemu kadhaa za Mpango wa EACOP.

## a. Tathmini kwa njia ya ushiriki na mijadala

EACOP imedhamiria kutekeleza tathmini kwa njia ya ushiriki na mijadala kwa viongozi wa mila na wana jamii kuhusu utekelezaji wa Mpango kazi wa EACOP kwa kutumia viashiria vifuatavyo. Viashiria hivyo pia vitakua sehemu ya mrejesho katika vikao vya mara nne kwa mwaka kwa viongozi wa mila na mikutano ya wana jamii. Viashiria vinaweza kuboreshwa ama kuongezwa kutokana na maoni yatakayo patikana katika mikutano ya mara nne kwa mwaka inayoendelea.

| Sehemu ya Mpango wa EACOP | Viashiria ama vigezo |
|---|---|
| Ushirikishwaji na ushiriki wenye uelewa | • EACOP huandaa mikutano minne kwa mwaka kwa viongozi wa mila.<br>• EACOP huandaa mikutano ya ngazi ya jamii, ikiwa ni pamoja na mikutano mahususi ya wanawake na vijana, angalau 75% ya wana jamii kila mwezi na 100% ya wana jamii kila robo mwaka. |
| Kujengeana-uwezo | • Mtoa mada mualikwa huongeza uelewa katika mikutano yote ya viongozi wa mila.<br>• Angalau mara moja kwa mwaka, mada ya ujengaji wa uwezo ijikite katika mada zenye umuhimu kwa wanawake.<br>• 100% ya nyaraka zinazo tumiwa na viongozi wa mila kwenye mikutano imetafsiriwa kwa Kiswahili (na lugha zingine za asili kama itakavyo ombwa).<br>• 100% ya washiriki wamewezeshwa kuhudhuria mikutano ya mara nne kwa mwaka. |
| Utatuzi wa Malalamiko | • Angalau mkutano wa mara moja kwa mwaka kufanyika kwa kila jamii kukuza uelewa wa namna ya utatuzi wa malalamiko.<br>• Mwakilishi wa PINGOs Forum kuhusishwa katika utatuzi wa malalamiko kwa malalamiko yote yanayo husiana na utekelezaji wa Mpango wa EACOP. |
| Kushughulikia Madhara | • Jamii zote hushirikishwa mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa katika maeneo yao kuhusu madhara na kujulishwa kuhusu mpango wa Kampuni katika kupunguza na kushughulikia madhara hayo.<br>• Mikutano rasmi ya wanawake na vijana huitishwa kwa kila jamii kujadili madhara yanayoweza kutokea na namna ya kushughulikia na kuyapunguza madhara ya kipaumbele kwa kundi husika mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa shughuli za ujenzi.<br>• Wakandarasi wote wakubwa na wadogo kufahamishwa kuhusu madhara yanayopewa kipaumbele pamoja na njia za kuepuka au kupunguza madhara hayo na namna ya usimamizi wake ndani ya wiki moja mpaka nne kabla ya kwenda katika eneo la kazi ili kuanza kazi. |

| Sehemu ya Mpango wa EACOP | Viashiria ama vigezo |
|---|---|
| Kuchochea manufaa ya kiuchumi. | • EACOP hukutana na kila jamii angalau mara nne kabla ya kuanza kwa shughuli za ujenzi katika maeneo yao ili kuwapasha habari wana jamii kuhusu fursa za ajira na taratibu za ajira.<br>• Asilimia 100 ya taarifa za fursa za ajira zina wasilishwa kwa jamii kwa njia ya nakala ngumu na pia kwa kutumia njia nyingine zitakazo kubaliwa na wana jamii kabla ya kuanza kwa michakato ya ajira.<br>• Mradi wa Uwekezaji katika jamii huundwa kwa kuwashirikisha viongozi wa mila na wana jamii na hufanikisha kuwepo kwa mkakati wa kutathmini utekelezaji.<br>• Viashiria vya nyongeza kwa kupima na kutathimini utekelezaji wa mradi wa uwekezaji katika jamii upo katika mkakati wa utekelezaji. |
| Ushirikiano na Serikali. | • Wawakilishi wa Serikali katika ngazi ya wilaya (DFP) hualikwa katika vikao vya viongozi wa mila. |

## b. Tathmini ya Mwisho wa Mwaka

Zoezi shirikishi la kila mwaka kutathmini utekelezaji wa Mpango wa EACOP utafanyika, kwa kuanzia, mwaka mmoja baada ya kusainiwa kwa Mpango wa EACOP. Njia kuu ya ushirikishwaji wa zoezi la tathmini utakuwa ukusanyaji wa maoni ambao utaundwa na kutekelezwa na NGO na washauri wa nje kama wataalam.

Maoni ya wanajamii yatawasilishwa kwa viongozi wa mila kama mrejesho wakati wa mikutano minne kwa mwaka karika robo ya pili ya mwaka 2023 na utafanywa hivyo katika ngazi ya jamii baada ya hapo. Matokeao ya maoni ya wana jamii yatawasilishwa na kujadiliwa na viongozi wa mila katika mikutano minne ya mwaka katika robo ya tatu ya 2023 na baadaye kwa viongozi wa jamii na wana jamii katika mkutano utakao fuata baada ya kukamilika kwa zoezi la kukusanya maoni.

Zaidi ya zoezi la mwaka la tathmini, Mpango wa EACOP utafanyiwa marejeo na kurekebishwa kama itakavyo onekana inafaa kuboresha utekelezaji wake. Nakala ya Mpango wa EACOP uliyo rekebishwa utasainiwa na uongozi wa EACOP na viongozi wa mila wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua Kama Watu wa Asili.

## Randama A: Wasifu wa Jamii

Baada ya Kukamilika, wasifu wa jamii utawekwa katika sehemu hii ya Mpango Kazi wa EACOP. Hivyo basi, hatua muhimu ni:

- Kujadili wasifu wa jamii na viongozi wa Mila wakati wa moja ya mikutano ya mwaka;
- Kuridhiwa kwa wasifu wa jamii katika ngazi ya jamii (ikiwa ni pamoja na madhara ya kipaumbele na namna ya kuyatatua) wakati wa utoaji elimu kuhusu tathmini ya Mazingira na Jamii unaofanywa na Asasi za Kiraia (NGOs);
- ukamilishaji wa wasifu wa jamii na kuambatanisha na mpango wa EACOP.

## Randama B: Nyaraka Rejea

Nyaraka zifuatazo zitakuwa Randama/zitaambatanishwa na Mpango wa EACOP:

1. Sera ya EACOP ya Haki za Binadamu
2. Chati ya Muongozo wa Usimamizi wa Malalamiko
3. Nyaraka za EACOP za Mawasiliano
4. MOU ya Asasi za Kiraia (NGOs) kuhusu utekelezaji wa Mpango wa EACOP

Mpango Kazi huu wa wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (Mpango Kazi wa EACOP) ni sehemu ya msingi kuhusu namna ambavyo EACOP ina shughulikia madhara yanayotokana na Mradi yanayoweza kutokea katika Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, kwa kuzingatia mila na desturi zao Pamoja na kuhesimu vigezo vya kitaifa na kimataifa kuhusu haki za binadamu, vikiwemo Vigezo namba 7 vya IFC kuhusiana na watu wa Asili.

Mpango huu wa EACOP umepatikana kutokana na umakini na ushirikishwaji kambambe na ambao bado unaoendelea kwa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili, mashirika yasiyo ya kiserikalli, wataalam wa kitaifa na wa Kimataifa na wadau wengine tangu mwaka 2017. Mpango huu umeundwa katika msingi wa Mfumo wa EACOP wa Jamii za Pembezoni Zinazojitambua kama Watu wa Asili (Mfumo wa EACOP) iliyo ridhiwa na kutiwa sahihi na EACOP Pamoja na viongozi wa mila wa jamii tajwa hapo yaani wa-Maasai, wa-Akie, wa-Bargaig Pamoja na wa-Taturu Octoba 2021.

EACOP - UK
GHOROFA YA 18, MTAA WA UPPER BANK NA. 10
UNITED KINGDOM E14 5BF

EACOP - UGANDA
COURSE VIEW TOWERS, KIWANJA NA. S2,
BARABARA YA YUSUF LULE
S.L.P. 34867

EACOP - TANZANIA
MSASANI PENINSULA KIWANJA NA. 1403,
KITALU NA. 1, NYUMBA NA. 7, BAINS AVENUE,
PEMBENI YA BARABARA YA CHOLE, SLP. 23139

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA© 2022
KIJARIDA HIKI AU SEHEMU YOYOTE YA KIJARIDA HIKI HAIRUHUSIWI KUCHAPISHWA, KUHARIRIWA, KUHIFADHIWA AU KUSAMBAZWA KWA NAMNA YOYOTE BILA YA KUWA NA IDHINI YA MAANDISHI YA UTAWALA WA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI – AFRIKA MASHARIKI.